

# MKATABA WA UPANGAJI

**MKATABA** huu umetayarishwa leo tarehe 12 mwezi 05 mwaka 2022

## KATI YA

**SALOME SANDRA** wa Dar es salaam Tanzania (ambaye katika mkataba huu atajulikana kama “**MWENYE NYUMBA**”) kwa upande mmoja.

NA

**LITTLE EGRET INVESTMENT COMPANY LIMITED** wa S.L.P 7224 Dar es salaam (ambaye katika mkataba huu atajulikana kama “**MPANGAJI**” kwa upande mwingine.

**NA KWA VILE** Mwenye NYUMBA amekubali kupangisha na Mpangaji amekubali kupangishwa sehemu ya nyumba (Chumba) hiyo kwa miaka **SITA** miezi **72** iliyopo Temeke kata ya **Chan'gombe**, Mtaa wa **Temeke**, Barabara ya **Mandela**, Namba ya kiwanja **123** Namba ya nyumba **123**. namba ya kitalu **D**  
**HIVYO BASI** Makubaliano hayo yameshuhudia yafuatayo

### 1. MUDA WA MKATABA

Mkataba huu utakuwa wa kipindi cha miezi **72** kuanzia tarehe **12** Mwezi **05** mwaka **2022** na utamalizika tarehe **12** mwezi **05** mwaka **2028**

### 2. KODI

Mwenye nyumba amekubali kupangisha na mpangaji amekubali kupangishwa katika sehemu hiyo ya nyumba kwa madhumuni ya kufanya biashara/ofisi kwa kulipa kodi ya shilingi (**500,000**) kwa mwezi mmoja. Wakati wa kutiliana saini mwenye nyumba amekubali kupokea **Tsh 6,000,000** ikiwa ni malipo ya miezi **KUMI NA MBILI TU**.

### 3. NI WAJIBU WA MPANGAJI KUTEKELEZA YAFUATAYO:-

- (a) Kutopangisha Mtu mwingine katika nyumba hiyo bila idhini ya Maandishi ya Mwenye nyumba
- (b) Kulipia gharama zote za umeme katika chumba hicho kwa kipindi cha Mkataba.
- (c) Biashara ya kamali, kilevi na vitu vya haramu vyote havitakiwi na kama kuna ukarabati mkubwa haurusiwi kufanya mpaka uwasiliane na mwenye nyumba.
- (d) Matengenezo madogomadogo anafanya mwenyewe pamoja na marekebisho yote madogo ya kuboresha.
- (e) Mpangaji anatakiwa kutoa taarifa mienzi miwili (2) kabla ya mkataba kumalizika kama anaendelea au haendelei.  
NB; kuvunja moja ya masharti haya utakuwa umevunja mkataba.

### 4. NI WAJIBU MWENYE NYUMBA KUTEKELEZA YAFUATAYO:-

- (a) Kuweka nyumba katika hali nzuri
- (b) Kutombughudhi Mpangaji wa chumba hicho anayesimamia kwa masharti yaliyopo.

**5. INAKUBALIWA PIA KUWA**

- (a) Endapo Mpangaji atakuwa na Nia ya kuendeleza atawajibika kutoa taarifa ya Maandishi ya mwezi mmoja kabla ya kipindi cha Mkataba kuisha.
- (b) Kama Mpangaji hatakabidhi nyumba hiyo kama walivyokubaliana basi Mwenye nyumba ana haki ya kumtoa kwa kutumia Dalali yeyote bila amri yoyote ya Mahakama.
- (c) Mgogoro wowote utatokea kuhusiana na Mkataba huu, basi mgogoro huo utatambuliwa kufuatana na sheria za nchi.

Mkataba huu umeshuhudiwa na wahusika kwa kutia sahihi zao katika namna na katika tarehe, mwezi na mwaka unaoonekana hapa chini.

UMESAINIWA na KUTOLEWA na  
SALOME SANDEA ambaye amekubaliwa  
Na ambaye namfahamu hapa Dar es salaam  
Leo 09 mwezi 05 mwaka 2022.

SD  
.....  
**MWENYE NYUMBA**

UMESAINIWA na KUTOLEWA  
Na **LITTLE EGRET INVESTMENT COMPANY LIMITED**  
ambaye amekubaliwa  
Na ambaye namfahamu hapa Dar es salaam  
Leo 09 mwezi 05 mwaka 2022.

瞿景辉  
.....  
**MPANGAJI**

SHAHIDI;

JINA DANIEL SIMON

SAHIHI [Signature]

ANWANI 105069 DSM.

KAZI WAKILI.



STAMP DUTY  
Tshs 60,000/= Collected  
Receipt No. 9981665989 Date 17/05/2022  
[Signature]  
Regional Manager - Ilala Tax Region

W.H.TAD 200000/=  
SD: 2 60,000/=  
660,000/=  
17/05/2022